SHULE YA SEKONDARI IKUWO

S.L.P. 113,

MAKETE

MOBILE 0782385397,0683807612

TAREHE: ……

JINA LA MWANAFUNZI: ……..

S.L.P. ……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IKUWO WILAYA YA MAKETE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Ninafuraha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha 1 katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Ikuwo ipo umbali wa km 42 kutoka Halmashauri ya wilaya ya Makete. Mhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11 Januari 2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 10 Januari 2021 kwa wasichana na endapo mwanafunzi aliyechaguliwa hataripoti kwa muda uliopangwa hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi/mlezi wa mwanafunzi husika.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE YA SHULE

WAVULANA

i.Suruali mbili : rangi nyeusi na rangi ya kijani jeshi ziwe na linda mbili mbele na mifuko mitatu, miwili mbele na mmoja nyuma,kitambaa kizito.
Mshono kata K au wowote usiofaa hauruhusiwi.
ii. Mashati mawili ya mikono mifupi rangi nyeupe.
iii.Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vya kufunga na kamba, vitavaliwa na soksi nyeusi wakati wote, yeboyebo(majagi) haviruhusiwi.
iv.Tai mbili: rangi nyeusi moja na rangi ya kijani jeshi moja.
v. Sweta lenye shingo “V” rangi ya kijani.
vi.T-shirt rangi ya bluu yenye nembo ya shule, itanunuliwa shuleni.

WASICHANA

i. Suruali mbili zitakazovaliwa na sketi: rangi nyeusi moja na rangi ya kijani jeshi moja. Kitambaa kizito koshibo.
ii. Blauzi mbili(mashati) rangi nyeupe mikono mifupi.
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vya kufunga na kamba, vitavaliwa na soksi nyeupe wakati wote , yeboyebo(bajaji) haviruhusiwi.
iv. Tai mbili , rangi nyeusi moja na rangi kijani jeshi moja.
v. Sweta lenye shingo “V” rangi ya kijani.
vi. T-shirt rangi ya bluu yenye nembo ya shule, itanunuliwa shuleni.

NB: Sare zote ziwe na heshima zinazoashiria maadili ya Mtanzania.

B. VIFAA MUHIMU

i.Daftari kubwa kumi(10) quire 4.
ii.Vitabu mbalimbali vya masomo ya sekondari (maduka ya vitabu watakusaidia kujua aina ya vitabu).
iii.Ndoo mbili za lita 10.
iv. Jembe moja lenye mpini.
v. Slasher 1(fyekeo).
vi. Mkebe (Mathematical set 1).
vii.Faili moja (flat file 1).
viii.Mfagio wa chelewa 1.

C. CHAKULA: KWA MWAKA

i.Fedha taslimu Tsh. 200,000/- kwa wanaolipa fedha tu.
ii.Fedha taslimu Tsh.100,000/- pamoja na debe 7 za mahindi na debe $1\frac{1}{2}$ maharage.

D. MAHITAJI KWA WASICHANA HOSTELI

i.Shuka mbili za light bluu.
ii.Blanketi nzito moja.
iii.Vyombo vya chakula.
iv.sanduku la chuma.
v.Taa au Torch ya betri/Sola.
vi.Godoro la nchi $2\frac{1}{2}$.
vii.Track suti 1 rangi nyeusi.
viii.Raba pea 1
ix.Nguo za kuogea vitenge viwili.
x.Shamba dress koshibo gauni rangi damu ya mzee 1.
xi.Nguo za ndani Chupi 7 na taiti 5.

3.1. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye Dhamana na elimu chini ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(night preparations).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(i) Kutunza mali za umma.

3.2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a. Wizi
b. Uasherati
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e. Kupigana au kupiga.
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g. Kudharau bendera yaTaifa.
h. Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i. Kutoa mimba.
j. Kugoma,kuchochea au kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k. Kukataa adhabu kwa makusudi.
l. Kuwa na simu ya mkononi.

4.0. MAMBO MENGINE YA MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

(a) "**Medical examination form**" ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara atakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubali sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/ MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

……

MKUU WA SHULE.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

P.O. – RALG

MAKETE DISTRICT COUNCIL

IKUWO SECONDARY SCHOOL

P.O. BOX 113, MAKETE.

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical Officer in respect of all form 1 entrants.

Full name: ……

Age: …….. Year …… Sex ……..

Blood count(Red and White cells) ……..

Stool examination ……..

Urine analysis ……

Syphilis Test ……

Eye test ……..

T.B. Test ……..

Ears ……

Chest ……

Spleen ……

Pregnancy test ……..

Abdomen ……..

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical or Chronic Disease of Family etc.

……
……..

I certify that the above person is fit to be a student.

Signature ……

Designation ……

Section ……

Date: ……

PUPIL

You must bring the form when you come to school. No pupil may be enrolled without certificate of physical fitness from the Doctor.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OR- TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

SHULE YA SEKONDARI IKUWO

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE NA MASHARTI YAKE

Mkuu wa shule

Shule ya sekondari Ikuwo

S.L.P. 113,

MAKETE.

A. MWANAFUNZI/MTOTO

Mimi ……. Nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule , pia sheria za shule. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninaahidi kutimiza wajibu wangu katika kufuata taratibu zote zilizopo ili niweze kufanikiwa katika kupata Elimu ya sekondari na kuendelea na elimu ya juu.

Sahihi ya mwanafunzi/mtoto …… tarehe ……

B. MZAZI/ MLEZI

Mimi …… Mzazi/mlezi wa …… ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Ikuwo nimesoma maagizo ya kujiunga na shule na sheria zake. Ninakubali nafasi hiyo na ninaahidi kumtimizia mtoto wangu maagizo yote ya kujiunga na shule katika muda uliopangwa.

Pia nitashirikiana daima na shule katika kumtunza na kumlea mtoto wangu ili aweze kufanya vizuri katika masomo yake.

Ahsante.

Jina la Mzazi/Mlezi ……..

Anwani ……

Kitongoji/Mtaa ninaoishi ……

Simu/Na. ya Nyumba/Kazini ……..

Tarehe …….. Sahihi ……